

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## KWANINI TUNAOGA JANABA?

لماذا نغتسل من الجنابة؟

HALIYAKUWA SIO NAJISI  
NA WALA HATUOGI KUTOKANA NA MKOJO NA HALI  
YAKUWA MKOJO NI NAJISI?

WAVEZA KUULIZA BAADHI YA WATU KWANINI  
UISLAM UMEAMRISHA KUOGA JOSHO LA JANABA  
HALI YA KUENEZA MAJI MWILI MZIMA HALI  
YAKUWA KIUNGO NI HICHO HICHO KIMOJA  
KINAHUSIKA KUTOA HAJA NDOGO NA MANII?

HEKMA KUBWA AMBAYO MOLA AMEONDOA JOSHO  
KATIKA HALI BAADA YA KUKOJOA NI KUTAKA  
KUWAONDOLEA WAUMINI UZITO KATIKA DINI'

HAKUNA ATAKAE BISHA KUWA KWA MWANADAMU  
MWENYE AFYA HAKOSI KWENDA HAJA NDOGO  
MARA ZISIZOPUNGUA KUMI KWA SIKU, TENA HII NI  
KWA MAKADIRIO YA CHINI BALI ANAWEZA KWENDA  
ZAIDI YA HAPO.

LAITI SHERIA INGEWEKA JOSHO KWA HAJA NDOGO INGEKUWA NI UZITO KATIKA DINI KWANI INGEMLAZIMU KILA ANAEKOJOA HAJA NDOGO BASI AOGJE JOSHO HALI AMBAYO HAJA NDOGO INAWEZA KUKUSHIKA MAHLA POPOTE WAKATI WOWOTE.

LAKINI JANABA UKIMCHUKULIA MWANANDO A HATA AFANYE TENDO LA NDOA MARA ATAKAZO WEZA BASI LINAMTOSHA JOSHO MOJA TU KISHERIA KWANI HAIJAFUNGAMANISHWA KUWA KILA TENDO LIWE NA JOSHO LAKE.

UKIMTAZAMA MTU ASIEKUWA KATIKA NDOA KWA YULE ALIYE BALEGHE JANABA LAKE ANAWEZA KULIPATA KWA NDOTO KISHERIA HALI AMBAYO SIO KILA SIKU ATAKUWA ANAOTA, HIVYO WAWILI HAWA WALIOLAZIMISHWA KUOGA JANABA UTAONA SIO MZIGO WALA UZITO KWAKUWA SIO KITU KINACHOJIRUDIA RUDIA MARA NYINGI KAMA MKOJO HIVYO NDIVYO SHERIA IKAWEKA KUOGA KWA MWENYE JANABA NA IKAWEKA KUTAWADHA KWA MWENYE KUKOJOA KWAKUWA KUOGA JANABA NI MWILI MZIMA HIVYO KUNAHITAJI TAKLIF KIDOGO HALI YA KUTAWADHA NI SEHEMU YA VIUONGO HIVYO KUTAWADHA NI WEPESI KULIKO KUOGA KWAKULE KUJIRUDIA RUDIA MARA NYINGI KULIKO YANAYOPELEKEA JANABA

KAMA ALIVYOSEMA MOLA KATIKA QURANI:

وما يريد الله ليجعل عليكم من حرج ولكن يريد ليطهركم وليتم نعمته عليكم تشكرون  
لعلكم

**MAANA YA AYA HII:** NA HAJAWA MWENYEZI MUNGU NI MWENYE KUTIA UZITO KWENU NYINYI LAKINI ANATAKA AKUTWAHARISHENI NA ATIMIZE NEEMA YAKE KWENU ILI MPATE KUSHUKURU.

ما قاله الإمام ابن القيم ردًا على من عجب من التفرقة بين المنى والبول فأوجب  
الغسل من المنى دون البول قال :

NA YAMENIFURAHISHA SANA MAJIBU YA IBN AL KAYIM ALJAWZIY ALIPO MJIBU MWENYE KUSHANGAA TOFAUTI YA JOSHO LA MANII NA MKOJO IKAWA NI WAJIBU KUOGA JOSHO KUTOKANA NA MANII HALI YA KUTOKUOGA KUTOKANA NA MKOJO .

AKASEMA:

هذا من أعظم محاسن الشريعة وما اشتملت عليه من الرحمة والحكمة والمصلحة، " فإن المنى يخرج من جميع البدن . ولهذا أسماه الله " سلاله " لأنه يسيل من جميع البدن فتأثر البدن بخروجه أعظم من تأثره بخروج البول.

NA HAYA NDIO YANAYOONYESHA UZURI WASHARIA YETU YA UISLAM NA YALIYOKUWEMO NDANI YAKE MIONGONI MWA HEKMA NA HURUMA PAMOJA NA MASLAHI,

KWANI HAKIKA YA MANII YANATOKA MWILI MZIMA NA NDIO MAANA ALLAH AKAYAITA "SULAALA" KWAKUWA YANA CHOMOZA KATIKA MWILI MZIMA HALI AMBAYO YANAUWATHIRI MWILI ZAIDI PALE YANAPOTOKA KULIKO UNAVYO ATHIRI MKOJO WAKATI UKUTOKA .

وأيضاً فإن الاغتسال من خروج المنى من أنفع شيء للبدن والقلب والروح

NA VILE VILE JOSHO LA JANABA NI LENYE  
KUUNUFAISHA ZAIDI MWILI, MOYO NA ROHO  
KUTOKANA NA ATHARI YA KUTOKA MANII.

فإنها تقوى بالاغتسال،  
والغسل يخلف على البدن ما تحلل منه بخروج المنى وهذا أمر يعرف بالحس

KWA HAKIKA MWILI UNAPATA NGUVU KUTOKANA  
NA JOSHO

NA JOSHO LINA FUATIA MWILI NA KURUDISHA YALE  
YALIO ONDOKA MIONGONI MWA NGUVU KWA  
KUTOKA KWA MANII.

NA JAMBO HILI LINAJULIKANA KWA KUHISI TU  
BAADA YA KUOGA JANABA NA KABLA PUNDE TU  
BAADA YA KUTOKA KWAKUWA KUTOKA KWA MANII  
KUNAUTIA MWILI UCHOVU NA UVIVU AMBAPO  
KUOGA KUNATIA NISHATI NA UCHANGAMFU,

HALI MKOJO UNAPOTOKA HAULETI UCHOVU WALA  
UVIVU HIVYO HAPA HITAJIKI JOSHO KAMA LA  
MWENYE JANABA.

اللهم اجعلنا من التوابين ، واجعلنا من المتطهرين

EWE MOLA TUJAALIE NI WENYE KUTUBIA NA  
UTUJAALIE KATIKA WATWAHARIFU (WASAFI)  
AMEEN!

Imekusanywa na Abubakar shabani Imepitiwa na Yunus kanuni